   Tamko la Yoshua lilikuwa nini katika mstari 15?

   _____

   Watu wote walitamka nini katika mstari 21? _____

   Watu walitoa ushahidi kwa ushuhuda walioambiana kumtumikia Bwana na kumtii. Kama jamii ilibidi watoe hesabu na kutoleana hesabu. Hii ilimaanisha katika mstari wa 23 kwamba jamii walipaswa kufanya _____

   _____

3. Yoshua alifariki. Tunaambiwa kuwa Israeli walimtumikia Bwana katika mstaeri 31. Je tunajua ni muda gani walimtumikia Bwana?

   _____

Mwisho Israeli walifika Kanaani . Uaminifu wa uwepo wa Mungu kwa muda wote wakiwa jangwani uliwafikisha watu wake katika nchi iliyoahidiwa muda mrefu. Nchi ni yao ya kumiliki. Mambo yangekuwa tofauti. Maisha ya jamii yangebadilika baada ya kila kabila kwenda kwenye eneo lake walilopangiwa. Kiongozi wao karibu atafariki. Maisha ya mbele yana wingi wa mashaka. Wageni bado waliendelea kuishi katika nchi na walipaswa kuangamizwa. Na sasa katka somo 4 tunasikia tamko la Yoshua la mwisho.

SOMO 4

Sehemu 1

KUTAFAKARI: Tuanfika mwishoni mwa maisha ya Yoshua. Waisraeli wanatumwa kwenye nchi waliyoimiliki na wako tayari kuanza maisha katika nchi yao. Yoshua anafariki katika umri wa miaka 110. Ameishi maisha zaidi na Mungu liko Mwisraeli yoyote isipokuwa Kalebu

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

Wosia wake unatukumbusha wosia wa Musa kwa watu kabla ya kufariki. Baraka na laana viliendelea kuwapo. Iwapo watu walichagua kutii, wangebarikiwa. Kama walichagua kutotii, wangelaaniwa. Yoshua aliwakumbusha kwasababu aliwafahamu watu. Alijua kuwa wangetumikia miungu mingine kutokana na uzoefu wa Mlimani Sinai. Alijua kuwa Mungu angeleta maafa juu yao hata baada ya kuwa mwema kwao. (Yoshua 24:20).

Kama wewe ni mdogo, huwezi kufahamu kwanini mzazi au babu anaongea maneno hayo kwako. Uzoefu wa maisha yao, umewafundisha mambo mengi. Hekim yao huzungumza na wale wanaowafuata. Ni mambo gani mtu mzima aliyokwambia unayokumbuka?

_____

Hekima wanayokushirikisha ni baraka yako. Je unaweza kukumbuka wakati uliposema "I remember." Kukumbuka ndiko kunakosaidia mambo ya nyuma yasikumbukwe. Ni mabo gani ambayo mtu alikuhimiza kukumbuka? _____

_____

Ni mambo gani unayofahamu ambayo ungetaka wengine wafahamu kuwa ni kweli kutokana na uzoefu wa maisha yako uliyokufundisha? ____

_____

KUKARIRI: Kifungu katika Biblia ni Yoshua 24:15. Kinasomeka, "Lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia Bwana (nyumba) familia, tutamtumikia Bwana." Hebu mstari huu utimize makusundi yake katika maisha yako wakati ukishuhudia kile unachoamini. Chukua dakika chache kuandika mstari huu mwishoni mwa kandi yako ukielezea matakwa yako kuwa na msimamo na kumtumikia katika kumshukuru kwa uaminifu wake kwako. Ameamua kuwa Mjungu wako na wewe kuwa mwana wake milele. Ameahidi mbingu kwa wote wanoamini kuwa Yesu ndiye anayetuwezesha kuwa watakatifu na washindi mbele za Mungu baba yetu. Kwasababu ya Yesu tunataka kusema "Lakini mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana!"

SALA : Nataka niwe jasiri kama Yoshua na kuwa na msimamo wa kukutumikia maisha yangu yote. Umekuwa mwaminifu kwangu. Niwezeshe kukutumikia kwa uaminifu. Mambu ya ulimwengu huu baada ya kutamani mambo mengi. Katika moyo wangu ninnajua machaguo haya huniweka mbali na wewe. Imarisha moyo wangu kutangaza huduma yangu kwako peke yako. Hasa nisaidie katika maeneo haya nikukiri wewe.

_____

UTANGULIZI: Yoshua amefariki. Hawana kiongozi. Hakuna mpango wa kurithiwa. Sura ya historia ya Israeli imefungwa. Ukombozi wao kutoka Misri, miaka arobaini ya msisha ya jangwani, kumiliki nchi ya ahadi imekamilika. Kabila zimegawanyika na kila kabila linasihi kwenye eneo walilopangiwa. Nchi imetulia kutokana na vita.

Walihitaji kiongozi sasa? Kusafiri hakukuwa tatizo tena. Walikuwa wamefika! Ni jambo gani litakalofuata? Maisha yao yalikuwa ni ya iuhamahama lakini sasa wametulia na kuweka mizizi katika nchi mpya. Hawawi tena tegemezi kwa kiongozi mmoja. Hawako tena katika msafara wa kikundi. Sasa waetawanyika mbali na kuishi kama makabila. .

Jambo la msingi la kukumbuka ni kuwa Mungu aliwaona kama watu wake wa agano, Kama jamii yake. Wote Musa na Yoshua waliwakumbusha juu ya baraka ambazo wangepata iwapo wangeishi katika kumtii Mungu. Aliwaambia pia matokeo ya kutotii sheria ya Mungu, laana ya uasi wao kama wangeabudu miungu mingine. Sheria ilikuwa imetolewa kwa Israeli kama watu wa Mungu. Sheria ilikuwa kile ambacho Mungu alitaka watii popote walipoishi katka nchi.

Sasa tunakaribia kujifunza Biblia kwetu kwa kutumia kitabu cha Waamuzi. Kutatokea nini kwa Israeli sasa kwamba hawana kiongozi tena na kwamba wana eneo kubwa la ardhi ambalo wanapaswa kumiliki?

Sehemu 2

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 1:19-36.

ZOEZI: Amri ya Mungu ilikuwa kuwa wote walikuwa katika nchi walipaswa kuangamizwa pasipo kubakiza mabaki. Pigilia mstari maneno yanayoelezea Waisraeli walichowafayia waliokuwa katika nchi.

Rejea	Waisraeli wachowafannyia walilkuwa katika nchi
Waamuzi 1:19	
Waamuzi 1: 21	
Waamuzi 1:25	

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

Waamuzi 1:27	
Waamuzi 1:28	
Waamuzi 1:29, 30, 31, 33	
Waamuzi s 1:34	

Waisraeli walivumilia badala ya kufutilia mbali. Wajadiliana na sheria ya Mungu katika kukamilisha kuchukua nchi. Wlikuwa na nchi kwa kabila lao. Walifurahi kwasababu waliowabakiza walikuwa vibarua wao. Kwahiyo kazi kubwa ilikuwa ni nini? Je wasingeishi pamoja kwa amani?

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 2:1-5.

ZOEZI:

- Malaika wa Bwana aliwaambia kuwa amefanya nini (mstari 1)?

  _____

- Walipaswa kufanya nini (mstari 2)?

  _____

- Walifanya nini hasa? _____
- Matokeo yangekuwa nini (mstari 3)? _____

  _____

- Watu waliitikiaje (mstari 4-5)? _____

Mistari hii inaonyesha chanzo cha tatizo lillowasumbua Israeli siku zote. Walikuwa na mashaka na nafasi yao siku zote, walishindwa kuchukua miliki yao. Sura ya pili yote ni ufupisho wa yaliyotokea baada ya kufariki kwa Yoshua.

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 2:6-23. Tazama majibu kwa maswali haya:

- Waisraeli walifanya nini katka maisha yote ya Yoshua?
- Vizazi vilivyofuata viliishije?
- Itikio la Mungu lilikuwa nini?
- Itikio la Israeli lilikuwa ni nini kwa Waamuzi ambao Mungu aliinua?
- Laana ya Mungu ilikuwa nini kwa watu?

ZOEZI:

1. Wati waliishije enzi za Yoshua (mstari 6-7)? _____

   _____

   Huu ulikuwa ni muda mzuri, muda wa amani kadiri walivymtumikia Mungu kwa uwezo wao. "Kwa kuona mambo yote Bwana aliyofanya kwa Israeli." Kisha Yoshua alifariki.
2. Lakini, habari inachukua muda mgumu. Imesemwa nini katika mstari wa 10?

   _____

   Swali la haraka lingekuwa: Kwanini kizazi kilichofuata hakikumjua Mungu au kwa yale aliyofanya kwa Israeli?

   _____

KUTAFAKARI: Tunavyosahau haraka. Mpaka tukumbushwe na kukumbuka tutasahau . Uzoefu wako ulikuwa ni nini?

- Kuna mtu aliyekukumbusha Mungu aliyoyafanya? Mtu huyo alikuwa ni nani?

  _____
- Kizazi kabla yako kilimjua Mungu? Uliambiwa juu yake? _____ Uliambiwa nini?

  _____

  Au, hukuambiwa kwahiyo hukufahamu upendo mkubwa wa Mungu kwako
  Kama ni hivyo, ni kumbukumbu gani ya kudumu ya maisha bila upendo wa Mungu?

  _____

Sehemu 3

ZOEZI:

1. Waamuzi i 2:11-12 inasema kuwa Waisraeli walifanya nini?
   - Walifanya _____ mbele za Mungu na _____ _____. (Hii ilikuwa miungu ya kigeni.)
   - Wali _____ Bwana ambaye _____
   - Wali _____ na _____ miungu mbalimbali.

2. Itikio la Mungu lilikuwa nini juu ya tabia yao (mstari 12-16)?

- Wali _____ Bwana ku _____.
- Kwanini? Kwasababu wali _____ Yeye na _____ _____ na _____.
- Bwana ali?
  - Mstari 14 _____ _____
  - Mstari 15 _____ _____

3. Mstari 16: Bwana aliinua waamuzi. Waamuzi walifanya nini? _____ _____

   Kumbuka: Waamuzi walikuwa viongozi, mara nyingi kama viongozi wa kijeshi ambao Mungu aliwainua kukomboa Israeli kutoka tawala za kikkatili wa maadui zao. Watu waliitikiaje waamuzi (mstari 17)? _____ _____

4. Elezea uhusiano ambao Mungu alikuwa nao na waamuzi _____

5. Kulitokea nini kati ya uhusiano wa Mungu ana watu wake (matari 20)? _____ _____

6. Mungu aliazimia kufanya nini (verses 21-23)? _____

KUTAFAKARI: Siyo picha inayovutia. Kwa uaminifu wa Mungu kwa waliokuwapo kabla ya kizazi hiki kilichosahauliwa na kudharauliwa. Uasi wake juu ya Mungu na kutotii agano lake amewasababisha kufanya zinaa na miungu mingine ya miti na mawe, mbele ya miungu ya wale ambao hawakuondolewa katika nchi, Baali, miungu ya Kisami, na mungu wa uzao. Wamekuwa mbali na Mungu wao anayewapenda, anayeokoa, na wamechagua utumwa na vifungo vya miungu mingine.. Walibadilisha vifungo vya mababu zao Misri kwa vifungo vyao vya kuabudu miungu mingine. Hawa miungu iliumbwa kwa hisia ya mawazo ya mwanadamu mwenyewe. Miungu yao ilikuwa haifai ambayo haikuwa na uhai wala pumzi, miungu ambayo ilitoa mauti. Musa na Yoshua waliwaonya kuhusu kumwacha Bwana Mungu wao lakini watu kwa ujasiri

walitamka, "Tutamtumikia Bwana" (Yoshua 24:21). Je walikumbuka? Wllikumbuka ahadi zao na kuzitunza?

MATUMIZI: Tunapoangalia maisha yetu wenyewe maisha yaw engine katika ulimwengu unaotuzunguka, tunaweza kujiuliza, "Tunakumbuka, au tumesahau?"

1. Ninajifunza nini Mungu aliyonifanyia? Ninakumbuka kuwa ameniumba? Kuwa amanita na kuniokoa, amenikomboa na kunifanya wake? Kuwa ameahaidi kuwa Mungu wangu na kunifanya kuwa mtu wake ? Ninakumbuka nini?

   _____

2. Je ninakumbuka kuwa ameniita ili niwe mtakatifu na asiyelaumiwa kwa damu ya Yesu iliyomwagika kwaajili yangu? Je ninakumbuka kuwa katika ubatizo wangu, kupitia katika maji, kuwa amenifanya mtoto wake na mrithi wa uzima wa milele? Nimekumbuka nini? _____

   _____

3. Je wale wanaonifuata wanajifahamu? Wanajua simulizi? Wanajua upendo mkuu kwao? Ninakumbuka yote Mungu aliyotenda kwaajili yao ili wasisahau? Ninaeza kukumbuka kuwaambia nini? _____

   _____

SALA: Chukua muda kuandika sala zao ilikuweke mawazo yako kwake. Mshirikishe shida zako kwaajili yaw engine ambao hawajasikia habari ya upendo wake mkuu. Walete watu mbalimbali wanaokuja kwenye mawazo yako na muombe aweke upendo ndani yako kuambia wengine aliyoyafanya.

Sehemu 4

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 3:1-5. Sura hii linaanza kwa kuorodhesha mataifa Mungu aliowaacha ili wajaribu Israeli ambao hawakuwa wazoefu wa vita. Mataifa yalikuwa: _____, _____, _____, and _____ (mstari 3). Kufuatana na mstari 4 kwanini Mungu alitaka kuwajaribu?

Waisraeli waliendelea kufanya nini (mstari 5-6)?

1. (mstari 5) _____
2. (mstari 6) _____
3. (mstari 6) _____

ZOEZI: Katika Zaburi 106:34-39 mwandika Zanuri anatoa ufupisho wa yale yaliyokuwa yakiendelea wakati huu wa historia ya Iraeli. Tena, si picha inayovutia. Kumbuka mistari hii sita ikituambia machaguo ambao Israeli walichagua:

1. Mstari 34-35: Ni matendo gani yaliyokuwa ya kutotii?

   _____

   Waliamua kufanya nin badala? _____

   _____

2. Vipi kuhusu miungu yao?
   a. Mstari 36: _____
   b. Mstari 37: _____
   c. Mstari 38: _____
3. Mstari 39: Walikuwa _____ wao kwa yale waliyo _____; kwa _____ wali _____wao.

FUNDISHO : Aina ya tabia inaanza kujifunua kama mwamuzi mmoja baada ya mwingine. Mapema katika somo hili tuliona katika Waamuzi 2:16-19. Mzunguko ulikuwa kama huu:

Waisraeli walifanya makosa wakaabudu miungu mingine (Uasi)

Mungu aliinua waamuzi ambao waliwaita kutubu (Toba)

Mungu aliwaokoa na maadui zao (Uokoaji)

Mungu aliwawezesha kuishi kwa amani na utulivu (Kupumzika)

Na mzunguko ulianza tena kadiri waisraeli walivyokuwa wafasadi zaidi ya mwanzo.

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

Kwasababu hatuwezi kwenda kwa undani kwa kila sura, tutaonyesha baadhi ya waamuzi na kukumbuka Israeli kama moja ya washiriki wa tabia au mwenendo. Unahimizwa kutumia kalamu ya rangi kuonyesha jinsi watu walivyokataa kuacha uovu wao na kiburi.

ZOEZI: Kwaharaka katika Waamuzi 3:7-11. Tabia fulani imeimarishwa.

- Waisraeli walifanya nini (mstari7)?
    - _____
    - _____
    - _____

    Walimsahau Bwana na kumbadilisha na miungu mingine. Mungu aliitikia nini kwa tabia zao (matari 8)?
    - _____
    - _____

    Alifanya Israeli wawe chini ya watawala wa kigeni.
- Waisraeli waliitikiaje kwa utumawa wao (mstari 9)?
    - _____

    Kutokana na kuishi kwa shida walimlilia Bwana.
- Mungu aliitikiaje (mastari 9)?
    - _____

    Mungu aliinua waamuzi waliowaokoa.
- Kulikuwa na _____ katika nchi hadi waamuzi _____(mstari 11).

Sehemu 5

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 3:12-16, 30 na waamuzi 4:1. Ni picha ya kusiktisha mstari 12 unaanza na maneno "*kwa mara nyingine*."

ZOEZI: Katika Biblia yako pigilia mstari kwa rangi tofauti, kwa kila sehemu zifuatazo katika mzunguko wa tabia ya wa Israeli .
Waisraeli walifanya nini?

1. Bwana aliitikia nini?

2. Kulitokea nini kwa Waisraeli?
3. Waisraeli walifanya nini?
4. Bwna alifanya nini?
5. Kulikuwa na hali gani mpya kwa nchi?
6. Kulitokea nini kwa waamuzi? Na , *mara nyingine.…*

Athanaeli, Elihudi, Debora na Gidioni wote walikuwa Waamuzi Katika Waamuzi 8:33-35 tunasoma kuwa mara tu baada ya kufariki kwa Gidioni kwa mara nyingine Waisraeli waliabudu Baali. Mtu anaweza kuuliza:

- Walikuwa wanavutiwa nini na miungu ya kigeni kiasi cha kujinajisi kwa kuiabudu? _____
- Kwanini wamwache Mungu aliyewakomboa kutoka mikononi mwa maadui zao wote (mstari 34)? _____ _____
- Kwa nini washindwe kuonyesha ukarimu wao kwa kiongozi wao kwa mema yote ambayo aliwafanyia (mstari 35)? _____

ZOEZI: Maneno na tungo nne hutuonyesha ni kwanini walifanya yale waliyofanya. Maneno hayo ni yapi katka mistari ifuatayo ?

1. Waamuzi 2:2 _____
2. Waamuzi 2:17 _____
3. Waamuzi 3:7 _____
4. Waamuzi 8:34 _____

MATUMIZI: Ujumbe huu unatupa maonyo pia. Tazama maneno haya yafuatayo, soma Agano la Kale kwa rejea ambayo yanawapa maelekezo Israeli, na soma rejea za Agano Jipya zinazotupatia maelekezo..

Maneno	Rejea za A. Kale	Rejea za A.Jipya
Tii	Kumbukumbu 6:5-6	Yohana 14:15, 23
Sikiliza	Kumbukumbu 30:20	Yohana 10:27-28
Usisahau	Kumbukumbu 4:9	Yakobo 1:25
Kumbuka	Zaburi 1 05:5	Luka 22:19

1. Tunaonyeshaje upendo wetu kwa Mungu? _____
2. Hatukuitwa kusikiliza tu bali kutenda pia _____
3. Ili tukumbuke tuliyoambiwatunashauriwa _____
4. Yesu anatoa nini ili tumkubuke? _____

_____

Kwa rejea hizi tumepewa mazoezi ya matendo kwa kufuata vizazi vitakavyofuata:

- Zaburi 78:5-7 _____
- Zaburi 145:4-7
  - Sema _____
  - Ongelea _____
  - Tafakari _____
  - Tangaza _____
  - Sherehekea _____

Unaweza kuimarishaje kumbukumbu yako ili usisahau ? _____

_____

Unaweza kufanya nini kuimarisha watu wengine ili wasije wafahamu kuwa Bwana hawasahau kabisa ? _____

_____

Somo 5

Sehemu 1

TUNACHOJIFUNZA KUHUSU MUNGU

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

1. Zaburi 106:40-46 tunakumbushwa juu ya hasira ya Mungu na ukali wake juu ya watu wake. Lakini chukua muda kuangalia kwa makini mistari 44-46. Pasipokujali uasi wao alisikia kilio chao na kwaajili yao ali _____ Agano lake
2. Zaburi 111:5b inatukumbusha tena kuwa Ali _____ Agano lake, si kwa muda bali _____! Kama alivyokumbuka agano aliloweka na Abrahamu, Anakumbuka agano alilofanya na sisi katika ubatizo. Ni Mungu wetu na sisi tu watu wake…milele!
3. Yermia 31:33-34 pasipokujali uovu anatusamehe maovu yetu hatusamehi tu, bali Ana _____ dhambi zetu. Anasahau dhambi zetu!

SALA: Bwana asifiwe, Ee roho yangu, na usisahau faida zake zote—anayekusahau dhambi zako zote na akuponye magojwa yako yote, aokoaye maisha yako kutoka shimoni akuvikaye taji ya upendo na rehema, ashibishaye matakwa yako kwa mambo mema ili ujana wako urejeshwe kama tai. Asante Bwana kwa kukumbuka agano la milele ulilofanya na watu wako. Asante kwa kusahau dhambi zangu, kwa kutozikumbuka tena. _____

KUCHIMBA KWA KINA: Kitabu cha Waamuzi kinatunza baadhi ya habari kuhusu Waamuzi ambao Mungu aliwainua kwa kufuata kifo cha Yoshua na na uzao wote ulimfahamu Bwana na aliyoyafanya kwa Israeli. Hawa waamuzi waliinuliwa kuwaokoa Waisraeli. Kutoka kwenye mikono ya waliowatesa japo Israeli hawakusikia waamuzi waliendelea kujinajisi juu ya miungu. Habari hizi nyingine si nzuri. Mfano mmoja umeandikwa katika Waamuzi 3, habari ya Ehud mkombozi wa mkono wa kushoto. Tukio lingine baya limetokea katika Waamuzi 4 wakati Debora akitumika kama Mwamuzi wa Israeli. Waamuzi 6 inaanza habari ya Mwamuzi mwingine mwenye nguvu Gidioni. Katika Waamuzi 11 tunasoma habari ya Yefutha, mtu aliyefanya kiapo cha uongo. Unahimizwa kusoma na kuanza kujizoeza na ukweli wa habari hii.

KAZI YA KUFANYA: Labda muhusika anayefahamika katika kitibu cha Waamuzi ni Samson, Mnaziri, mtu anayejulikana kwa nguvu zake na uovu. Habari inaanzia katika Waamuzi 13. Unaposoma onyesha mambo yafuatayo:

- Wahusika katika habari hii

- Tatizo
- Ukweli katika Wanaziri
- Kukutana na malaika wa Mungu
- Sala zilizojibiwa

ZOEZI:

- Nani aliyewaongoza Waisraeli? Kufuatana na mstari wa 1 kwanini haya yalitokea?

  _____

- Ni nani mhusika wa kwanza katika habari? _____
- Shda ilikuwa ni nini? _____
- Pamoja na shida ya mwanamke, ujumbe wa malaika kwake ulikuwa nini?

  _____

Sehemu 2

FUNDISHO: Nani alikuwa mnaziri? Wanaziri walikuwa watu "waliotengwa." Malaika wa Bwana alitoa maelekezo mahususi amabayo yangefanyiwa kazi mara moja na aliendelea na mimba. Maelekezo haya yalikuwa yapi (mstari 4 na 5)?

a. _____
b. _____
c. _____

- Maelekezo haya yaliimarishwa tayari katika Hesabu 6:1-21. Linganisha masharti na maelekezo ya Wanaziri na maneno yaliyosemwa na malaika wa Bwana katika Waamuzi 13:3-7. _____

  Mnaziri alikuwa ni mtu aliyetenga kwaajili ya Bwana. Uwepo wake ulikuwa kama kumbukumbu inayoonekana kwamba Mungu ameita watu wake katika utakatifu kwa kujitenga kutoka kwenye miungu iliyowazunguka na kuishi wakiwa wametengwa kama watoto wa agano la miele.

ZOEZI:

1. Ni yapi yalikuwa maombi ya Manoa? Maswali yake yalikuwa yapi? (mstari 8)

   _____

2. Manoa anakaribisha wageni na kula pamoja nao. Kisha anamuuliza malaika wa Bwana, "JIna lako ni nani?" JI lilikuwa lipi? _____
3. Kisha, malaika wa Bwna alijitambulishaje mstari 19-21? _____

   _____
4. Itikio la Manoa na mke wake lilikuwa nini (mstari 22-23? _____

   _____
5. Bwana alitunza agano la Manoa na mke wake. Samsoni _____ na Bwana _____ yeye, na _____ alianza ku _____

KUTAFAKARI: Chochote tunachoweza kumwambia huyu mtoto ni cha pekee. Alizaliwa na mwanamke aliyekuwa tasa na hana mtoto mwingine. Maisha ya Samsoni yote angekuwa mnaziri, aliyetengwa kawaajili ya Mungu. Wazazi wake walikuwa wacha Mungu wakiomaba Mungu awafundishe jinsi ya kumlea mtoto na kumomba kufahamu ambayo yangekuwa masharti ya mtoto katika maisha yake na kazi yake. Waliamini waliyoambiwa na kuyatendea kazi.

Wazazi walisoma kila mara vitabu vilivyomwambia mama matarajio yake wakati wa mimba au mtoto angetaka nini mara baada ya kuzaliwa na malezi yake toka hatua moja kwenda nyingine katika kukua kwake. Wazazi katika Waamuzi 13 walikuwa na wasiwasi tofauti. Walimwomba Mungu awafundishe jinsi ya kulea mtoto ambaye angezaliwa. Kama ungekuwa ni wewe uliyetarajia kuwa mzazi ungemuomba nini Mungu? _____

_____

ZOEZI: Ni maelekezo gani yametolewa katika kila mstari?

- Mwanzo 18:19 _____
- Kumbukumbu 6:5-9 _____

  _____
- Methari 22:6 _____
- Waefeso 6:4 _____

Sehemu 3

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

MATUMIZI: Kama aliyetarajia kuwa mzazi alikuwa hana mme wala mtoto, Manoa atafuta maelekezo namna ya kuishi maisha.

1. Ina maana gani kwangu kutengwa kwaajili ya Mungu?

   _____

2. Kwa kudhani kuwa bado kuchelewa, ninahitaji mafundisho na maelekezo gani katika maisha yangu yaliyobaki? _____

   _____

3. Ni tamko? _____

   _____

SALA: Andika sala yako ukiomba Mungu akuongoze katika maisha ambayo ungeendea

_____

UTANGULIZI: Mwisho wa Waamuzi 13 tulidhani tuna mtoto mkamilifu, mtoto aliyependa na kuheshimu wazazi wake, mtoto aliyekua kama aliyebarikiwa na Bwana amabaye ndani yake Roho Mtakatifu aliishi. Sura 14 inaanza kwa kutuambia juu ya maisha ya huyu mtoto ambaye sasa ni mwanamume. Tunapoendelea kujifunza juu ya maisha ya Samsoni weka mawazoni makusudi ya kumtenga Samsoni. Mwisho wa Waamuzi 13:5 inatwambia kuwa "ataanza _____ _____ kutoka kwenye mikono ya _____".

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 14. Angalia kwa:

- Samsoni alitaka nini?
- Mabishano yalihusu nini?
- Kulitokea nini katika njia ya Timnah?
- Kumbuka tukio la mzoga na asali.
- Kulitokea nini kwenye sherehe?
- Habari inamalizikaje?

ZOEZI:

1. Ikiwa kwenye mawazo kuwa Samsoni ataaza kuokoa Waisraeli kutoka kwa Wafilisti, soma sura yote ya 14 kwa mara nyingine onyesha *ukwel*i muhimu wa habari.

- _____
- _____
- _____
- _____
- _____

Andika ukweli wa nyongeza katika daftari yako.

2. Samsoni alikuwa anadai kuwa wazazi wake _____ mwanake kama mke wake (mstari 2). Kwanini wazazi wake walikataa kwa nguvu ombi lake?

   _____

3. Roho wa Mungu alikuja juu yake kwa nguvu. Hii ilikuwa mara ya kwanza nguvu zake za kimwili zilipoonekana. Kulikuwa na umuhimu gani kwa asali kutoka kwenye mzoga wa simba ? Unakumbuka nini kutoka Hesabu 6:6-7? _____

   _____

4. Mke wa Samsoni alitishwa na wasindikizaji. Walitishia kufanya nini (mstari 15)?

   _____

5. Kwahiyo mkwa wa Samsoni anakwenda nyumbani na kulia kuomboleza na kuenelea kumsihi Samsoni kiasi cha Samsoni kushindwa kujisisimamia. and then sob and whine and continues to press Samson until he can stand it no longer. Alimfichulia siri yake. Matokeo ya kumpa jibu mke wake yalikuwa ni nini ? _____

   _____

6. Samsoni alijua jinsi walivyopata majibu kwasababu ni Delila peke yake alifhamu. Majibu ya Samsoni yalikuwa nini kwa majibu yao? _____
7. Kwa mara nyingine, Roho wa Mungu alikuja juu yake kwa nguvu (mstari 19). Alifanyaje?

   _____

   Samusoni alikasirika. Alikwenda wapi? _____
   Kulitokea nini kwa mke wake?

   _____

8. Ulitarajia kuwa habari itaishaje? _____

   _____

Sehemu 4

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

TUNACHOJIFUNZA KUHUSU MUNGU:

- Mwanzoni mwa sura hii Samson anaelezewa kama mtu mgumu asiye na utii. Alikataa kufuata sheria ya Mungu ili aoe mwanamke wa Kiebrania tu. Badala yake alilazimisha kuoa mwanamke wa Kifilisti. Tena tunasoma katika mstari wa 4: "Wazazi wake hawakufahamu kuwa hii ilikuwa ikitoka kwa Mungu, aliyekuwa akitafuta nafasi ya kuwakabili Wafilisti…" Na tunauliza tena. Haya yalikuwa mapenzi ya Mungu? Hii ina maana kuwa Mungu mara nyingine Mjungu anafanya mtoto kuwa mkaidi? Au hii inamaanisha kuwa Mungu anaweza kujanga mazingira ambayo yanaweza kumfanya kutimiza malengo yake matakatifu? _____

  _____

- Mara mbili katika sura nii tunasoma kuwa "kuwa Roho wa Mungu alikuja juu yake kwa nguvu." Mara nyingi Samsoni alionyesha nguvu isiyo ya kawaida. Tukio la kwanza linasemwa katika sura ya 5-6 na la pili lilikuwa katika sura ya 19. Moja alikuwa akipambana na _____ na nyingine alikuwa _____. Mungu alichagua Samsoni kuonyesha nguvu yake. Kumbuka ulipoona nguvu za Mungu zikidhihirika kupitia mtu mwingine. Kutumia nguvu nyingi kuliko kawaida ni njia nyingine inayoonekana wakati wa dharura au hatari wakati mwingiene inaposababisha kuvunja miamba.
- Je nguvu kama hizi humaanisha nguvu za kimwili? Tunajifunza nini juu ya Mungu tunapoambiwa kuwa Roho wa Mungu alikuja juu yake kwa nguvu? _____

  _____

FUNDISHO: Inawezekana huna uzoefu wa nguvu ya Mungu. Samsoni alikuwa mtu asiye wa kawaidaa. Si kwamba aizaliwa na mwanamke ambaye alikuwa tasa tu bali alitengwa kama mnaziri Alizaliwa kwenye familia ya ki Mungu ambao waliliitia jina la Bwana walipomlea mtoto kwa kazi ambayo Mungu alikuwa amempangia kufanya.

Inawaezakana ukawa unashangaa: Kama sijawa na uzoefu wa Roho wa Mungu, inawezekana kuwa ninatatizo fulani? Roho wa Mungu siyo hisia. Si kusubiri tukio la hisia na jaziba. Roho wa Mungu anakuja juu yetu katika hali ya kawaida. Kuleta upendo kwa mtu mpweke, rafiki

anaye umia, kusikiliza kwa makini kwa aliyekata tamaa na hofu kwa mtu aliyepoteza kazi au kukosa kupandishwa cheo, na kusherekea ukamilifu, kuzaliwa au uchumba vyote ni mifano ya hali ya kawaida ambayo Roho wa Mungu huja kwa nguvu.

Kwa wale ambao wamekuwa watu wake kwa njia ya ubatizo, Roho wa Mungu huja kwa nguvu pale anapowadai kuwa wake. Anawatenga kwa makusudi yake matakatifu. Matumizi ya maji ya kawada na Neno lake takatifu huungana kutupatia uzoefu usio wa kawaida. Katika ubatizo anatufanya watoto wake, warithi wa ufalme wake na hutoa uzima wa milele pamoja naye. Katika ubatizo anachukua uchafu wa dhambi zetu na kutupatia kipimo cha neema na huruma yake kisicho cha kawaida kwa msamaha wa dhambi zetu zote. Kama huna uzoefu wa neena na huruma yake isiyo ya kawaida, msamaha wa dhambi zako zote kwa njia ya imani kupitia Yesu, maombi yangu kwako ni kuwa Roho wa Mungu atakuja juu yako kwa nguvu kwa muda huu.

SALA: Ee Yesu, Ulikufa kwaajili yangu. Wewe ni mwokozi wangu. Roho wako aje juu yangu kwa nguvu ambayo inakuja kwa kukufahamu. Niepushe na kutafuta nguvu zisizo za kawaida zilizojaa jaziba na hisia badala yake fungua macho yangu kuona Roho wako akiwa katika kazi kwa hali ya kawaida katika njia u nayochagua kunitumia. Leo ninaleta maombi yangu maalumu yenye sifa na shukrani kwa Baraka ambazo kwa neena umeweka katika maisha yangu.

MARUDIO: Tayari katika Waamuzi 13, hata kabla ya kuzaliwa kwake, tunajifunza kuwa Samsoni alikuwa amepangiwa kuwa mnaziri, aliyetengwa kwaajili ya Mungu (tazama mstari 5) na kwamba angeanza ukomnozi wa Israeli kutoka kwa Wafilisti. Katika Waamuzi 14:2 tunajifunza kuwa Samsoni aliamua kuoa mwanamke Mfilisti. Mwanamke huyu ni njia ambayo Mungu alichagua kuwakabili Wafilisti (Waamjuzi 14:4). Kwavyovyote vile, katika hasiria yake Samsoni alirudi nyumbani kwa baba yake na mke wake alitolewa kwa rafiki ambaye alimuhudumia wakati wa harusi yake.

Sehemu 5

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 15. Kwa mara nyingine utaona ukweli wa simulizi

- Samsoni alijifunza nini aliporudi kwa mke wake?

- Kisasai cha Samsoni kilikuwa nini?
- Nini lilikuwa itikio la Wafilisti?
- Waisraeli walihusishwaje?
- Mungu aliitikiaje kwa hitaji la Samsoni?

ZOEZI:

1. Kulitokea nini wakati Samsoni alipokwenda kwa mke wake Mfilisti (mstari 1-2)?

   _____

2. Baba wa mwanamke alisuruhishaje tatizo? _____
3. Samsoni alihisi kuwa kisasi chake kwa Wafilisti kilikubaliwa. Aliamua kufanya nini (mstari 4-5)? _____
4. Wafilisti waliitikiaje (mstari 6)? _____
5. Itikio la Samusoni lilikuwa nini (mistari 7-8)?

   _____

6. Mwamba wa Etamu ulikuwa katika himaya ya kabila laYuda. Ili kumkamata Samusoni. Wafilisti waliweka kambi Yuda. Yuda alifanya nini mara tu baada ya kufahamu kuwa Wafilisti walichotaka kufanya (mstari 11-13)?

   _____

7. Kwa mara nyingine kulitokea nini katika mstari wa 14?

   _____

8. Inaonekana kuwa kisasi cha Samusoni kwa Wafilisiti kilikamilika. Aliridhika. Mahali pale paliitwa. _____
9. Samusoni anahitaji la kweli mstari 18. Ni nini?

   _____

10. Waba aliitikiaje? _____
    Samusoni aliimarishwa tena na kupewa nguvu mpya.
11. Israeli ilikuwa chini ya utawala wa Wafilisiti. Samusoni, kwavyovyote alitumika kama Mwamuzi na aliongoza Waisraeli katika kipindi hiki. Kwa muda gani?

    _____

FUNDISHO: Sura hii inahusu kisasi. Kisasi kinatokea kwaajili ya mtu mmoja au kikundi. Kisasi ni kama tamaa isiyoridhika. Haitosheki. Kisasi ni kujaribu kupata juu ya mkono. "Ni

muda kurudisha! Nitarudisha mapigo. Nitakurudishia." "Sitaacha ipite bila kulipa kisasi." "Ulinisababishisa maumivu nitaona unapata maumivu yale yale." Na malipo kwa kawaida ni mabaya kuliko ya kwanza. "Sitatulia hadi nitakapoona kuwa umepata kile unachostahili." Inaonyesha kuwa nina haki nawe una makosa.

SWALI LA CHANGAMOTO: Dawa ya kulipa kisasi nini na inapatikana wapi? _____

_____

SOMO LA 6

Sehemu 1

TUNACHOJIFUNZA KUHUSU MUNGU: Mistari hii inatwambia nini kuhusu kisasi cha Mungu?

- Kumbukumbu 32:35 -

  _____

- Isaya 2:12, 17-18 - _____

  _____

- Mambo ya Walawi 19:18 -

  _____

- Warumi 12:17-21 - _____

  _____

Andika ufupisho wa maneno. Tunajifunza nini kuhusu Mungu na kisasi kutoka katika kifungu hiki?

_____

MATUMIZI: Lazima tuchukue muda kukumbuka mwitikio maovu yanayofanyika kwetu au ni kwa makusudi au la. Mambo yasiyo haki yanatokea kila siku. Mambo mengine yanaonekana kuwa mabaya. Baadhi ya matendo na mwitikio si sahihi. Tunaitikiaje? Samsoni aliona kuhesabiwa haki kwa kulipa kisasi kwa mabaya yaliyofanyika kwake na Wafilisti na kinyume chake. Kutokana mafunzo yetu tumejifunza nini kwa mwitikio wa komungu wa kulipa kisasi. ?

_____

Kuna jambo lisilo haki linalokua katika mawazo yako, wakati mwingine iliyofanywa na wewe au kwako. Maelekezo ya Mungu nin kwa kuishi maisha kama hayo?

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

Ni wakati gani unaona shidha kuitikia kimungu katika hali ya kutotenda haki?

Magazeti yamejaa habari za watu wanaolipa visasi wengine. Juma lijalo tafuta mada ya magazeti inayohusu malipizi. Tunaweza kujifunza nini kuhusu matukio haya?

KUKARIRI: Soma Zaburi ya 94. Malipizi ni kazi ya Mungu. Mungu ni kama mwamuzi. Ndiye gome na mwamba wetu, mahali tunapoweza kukimbilia na kujificha. Samsoni alikimbilia kwenye pango la Etam. Bwana Mungu ni mwamba tunaoweza kukimbilia. Atalipa kisasi na kuharibu waovu. Hii ni ahadi yake Andika Zaburi 94:1-2, 22-23 kwenye kadi. Ikariri! Ishike kadi mikononi na ukumbuke ni mara ngapi wewe mwenyewe ulipotaka kulipa kisasi.

Sehemu 2

FUNDISHO: Kushughulika na visasi sawa na Mungu ni juu ya uwezo wetu wa kibinadamu. Matakwa yetu ni kulipa mabaya kwa mabaya. Yesu mwenyewe alitupa gharama ya mwisho kwa kutolipa baya kwa baya. Tazama rejea hizi na kumbuka ukweli ambao mifano hii inafundisha.

References	Teaching
Mathayo 5:44-45	
Luka 23:34	
Matendo Acts 7:59-60	
Warumi 12:14-21	
1 Petro 2:23-24	
1 Petro 3:9	

Andika ufupisho wa tunachojifunza kutokana na rejea katika kuitikia wale wanaotutenda mabaya.

SALA: Ee Bwana, mara nyingi najikuta katika hali ya kuona kuwa wenzangu wamenitendea isivyostahili. Lazima ulijisikia hivyo uliposulibishwa msalabani. Ulifanya nini kiasi cha kupata

adhabu hiyo hadi mauti? Ulikuwa kimya. Haukutafuta kisasi. Hukumwomba baba kulipa baya kwa baya. Ulinyamaza kwaajili yangu. Nipe kipimo cha ziada cha nguvu yako. Nguvu ya Roho wako iwe juu yangu, Bwana, badala ya kulipa visasi wengine niko tayari kupenda wengine sawa na ulivyonipenda. _____

_____

UTANGULIZI: Waamuzi 16:1-22 inaanzia na kuishia Gaza, Mji ulio kusini mwa himaya ya Filisiti. Onyesha mji huu kwanye ramani kupita pwani ya Bahari ya Mediteraniani Magharibi mwa Bahari ya Chumvi. Habari ya Samsoni na Delila inaonyesha udhaifu wa mwanamume huyu kwa dhambi. Kumbuka Mungu amempa maelekezo Manoa na mke wake kwamba mtoto wao Samsoni hakupaswa kunyoa nywele zake. (Waamuzi 13:5).

Jambo lingine la muhimu la kukumbuka ni kwamba Samsoni kama manaziri alilikuwa ametengwa kuanza ukombozi wa Waisraeli kutoka kwa Wafilisiti. Tunajifunza kuwa kwa mara nyingine Waisraeli walitenda maovu machoni pa Bwana ambaye aliwakomboa kutoka mikoni mwa Wafilisti (Waamuzi 13:1). Wafilisiti walikuwa tishio kwasababu ya uwezo wao wa ziada wa kutumia chuma. Kwa muda mrefu watu hawa walikuwa tishio kwa Israeli. Yalikuwa mabaki ya waliomiliki nchi ya ahadi wakati Israeli walipoanza kuchukua maeneo yao. Kwahiyo wakati wa utawala wa Samsoni waliendelea kuwa tishio kwa Israeli.
Uhusiano wa Samsoni na Delila umezoeleka. Pamoja na hayo watu wengi hawafahamu kuwa Samsoni alikuw ametengwa kwaaji ya makusudi ya Mungu matakatifu. Unaposoma habari kumbuka uhusiano wa wahusika hawa wawili na kumbuka kama huu ni upendo wa kweli au hapana.

KAZI YA KUFANYA: Soma Waamuzi 16:1-22. Angalia *ukweli* wa habari.

- Wahusika wa simulizi ni aki na nani?
- Hila ni ipi?
- Habari inaishaje?

Sehemu 3

ZOEZI:

1. Watu wa Gaza Wafilisti wameandaliawa kukamilisha nini (mstari-2)?

   _____

   a. Samasoni alikuwa ni nani?

      _____

   b. Alijifichaje (mstari 3)? _____

      _____

2. Delila ni mpenzi mpya katika maisha ya Samsoni (mstari 4). Alikuwa mjanja na mjanja. Ni mpango gani aliokuwa amekubaliana na viongozi wa Wafilisiti (mstari 5)?

   a. Angefanya nini? _____

   b. Malipo yake yangekuwa nini? _____

3. Mara tatu Delila alimsihi Samsoni amwambie siri ya nguvu zake akimdanganya. Angalia maenedeleo ya mwenendo wa ujanja wake:

   a. Mstari 6:

      _____

   b. Mstari 10:

      _____

   c. Mstari 13:

      _____

   Delila alikuwa mvumilivu kwa ujanja wake kwa faida yake binafsi.

   Kwa mara tatu Samson alimpa majibu ya utani

   d. Mstari 7:

      _____

   e. Mstari 11:

      _____

   f. Mstari 13:

      _____

   Samsoni alifurahia kuficha siri ya nguvu ya siri yake kwa Delila.

4. Mashitaka ya Delila yalikuwa ni yapi (matari wa 10, 13, 15)?

   _____

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

5. Delila alitumia mbinu gani kugundua nguvu zake za ajabu (mstari 16)?

   _____

6. Kwa ushawishi na ujanja mwingi Delila alifanikiwa. Alipata taarifa alizotaka, aliwaambia viongozi wa Wafilisti ambao wakuja mbio na malipo ya fetha, wakakata nywele zake wakati amelala, na _____(mstari 19).
7. Kulitokea nini Samsoni alipozinduka (mstari 20)?

   _____

   a. Wafilisti walimkamata. Walimfanyia nini ? _____
   b. Walimpeleka wapi? _____
   c. Walimfanya afanye nini? _____

8. Mstaro wa 22 unaonyesha dalili ya matumaini? _____

   _____

KUTAFAKARI: Mtu hawezi kusaidia ila kuuliza maswali: Ni jambo gani lililoharibika? Hapa kuna mtu aliyekuwa na nguvu zisizo za kawaida, mtu aliyetengwa kwaajili ya Bwana tangu kuzaliwa, aliyeongoza Waisraeli kwa miaka ishirini, aliyekuwa aanze ukombozi wa Israeli kutoka katika mateso. Sasa mtu yuleyule ni dhaifu, kipofu, na amepewa kazi ya kusaga garezani. Mtesi aliyetumwa amwangamize inaonekana anamwangamiza yeye.

Hatimaye tabia ya Saomsoni ya kutotawala tabia yake ya ngono ilimuingiza hatarini. Alidai wazazi wake wampe mwanamke Mfilisti (Waamuzi 14:2). Alimchukua malaya (Waamuzi16:1) na sasa ameingia kwanye mapenzi na mwanamke mwingine (Waamuzi 16:4). Serious Matokea makubwa yalifuatana na kila tukio. Kwa mke wake ilikuwa ni kitendawili na matokeo ilikuwa kutoa majoho therathini na jozi za nguo. Kwa malaya ilikuwa ni kuhusu watu wa Gaza wakijaribu kumuua na malango ya mji yaliharibiwa, na kwa Delila nguvu zake ziliondoka na Bwana alimwacha. Mtu huyu angejifunza nini zaidi kwa ujinga wa mwenendo yake?

Kwa njia nyingi Samson anaonekana kuwa kama mtoto aliyepewa mwili na nguvu anayeishi kwa ujinga kama mtoto asiye na nidhamu na ukomavu. Hamu yake ilidhihidhirisha matendo

yake. Matokeo yake ni anahatarishwa na tamaa yake akakosa hekima ya kujibu wakati wa kujaribiwa.

Hautuwezi kuuliza chochote bali kushangaa kile alichokuwa akifikiri kwa muda huu wote alipokuwa akisanga na ngano akiwa gerezani. Kama ungepata muda wa kumuuliza Samsoni akisaga, ni maswali gani matatu ungetaka kumuuliza? Maswali yako hayapaswi kujibiwa kwa "ndiyo" au "hapana." Maswali yako hayapaswi kuanza na "kwanini?"

- _____
- _____
- _____

Sehemu 4

MATUMIZI: Hatuwezi kuhoji maisha ya Samsoni tusipohoji maisha yetu wenyewe. Fikilia yale amabayo yamekuungiza hatarini kutokana na uamzi wako usio na busara. Kumbuka tamaa zako za mwili zinazodhihirisha udhaifu wako: _____

_____

Unasikia zikikuambia nini zinapokuangusha kwa kukuwaka na kukutesa?

_____

Zinakuletea mashtaka gani ya uongo na upumbavu? _____

_____

Nguvu yako iko wapi unapobambana na majaribu ya tamaa? _____

_____

ZOEZI: Tukitazama upande wa nguvu yako peke yake, tunashindwa kuona nguvu ya Mungu. Mistari hii inatufundisha nini kuhusu nguvu ya kweli?

Rejea	**Fundisho**
Kutoka 15:2	
2 Samwel 22:33	
Zaburi 46:1	
Isaya 40:31	

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

1Wakirintho 1:25	
1Petro 4:11	

KUKARIRI: Wafilipi 4:13 ni mstari mfupi kwa kukariri. Pamoja na hayo mstari huu hubeba ukweli. Unatukumbusha kuwa tunaweza kufanya kila jambo, hata tukikumbana na magumu. Neno "kila jambo" linaunganisha kila kitu. Mwanzo wa kila jambo ni Mungu. Ninaweza kufanya mambo yote katika yeye! Ni mtoaji wa nguvu zote. Ni Yeye anipaye nguvu. Kwa mara nyingine unahimizwa kuandika kifungu hiki katika kadi. Furahia zoezi la kukikariri. Jizoeze kuwa karibu na nguvu ya Bwana hata ikiwa ni kimwili, kiakili, mawazo, hisia au kiroho.

SALA: Andika sala yako ukitumia Waefeso 3:16 na Wakolosai 1:11. Badilisha viwakilishi kwa kuifanya kuwa yako. Mungu angetaka kusikia ukitumia Neno lake ukizungumza naye; ni sawa

_____

KAZI YA KUFANYA: Samasoni alikamatwa; macho yake yalitobolewa, na sasa Wafilisti wako naye Gaza gerezani akisaga. Waamuzi 16:22 inasema kuwa nywele zake zilianza kuota tena. Nguvu zake zilianza kurudi. Soma Waamuzi 16:23. Tafakari yafuatayo:

- Kwanini Wafilisti walikuwa wakisherekea?
- Viburudisho vyao vilikuwa ni nini?
- Maombi ya Samsoni yalikuwa ni nini?
- Mungu alijibuje maombi ya Samsoni?

ZOEZI:

1. Viongozi wa Wafilisti waliamua kufanya nini (mstari23)?

   _____

2. Watoa nini kwa kumkamata Samsoni? _____
3. Kisasi chao kilitimizwa. Samsoni alifanya nini kilichomfanya awe adui yao (mstari 24)? Rudia rejea hizi:
   a. Waamuzi 14:19 -

      _____

   b. Waamuz 15:3-5 -

      _____

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

c. Waamuz 15:14-15 -

_____

4. Umati ukila na kucheza sasa walimwita Samsoni. Walitaka afanye nini (mstari 25)?

_____

5. Samsoni alimwomba muhudumu afanye nini (mstari 26)?

_____

6. Tunajifunza nini kuhusu hekalu la Dagoni mstari 27? Nani waliokuwa wamekusanyika kuangalia kazi michezo wa Samsoni?

_____

7. Maombi ya Samsoni yalikuwa nini (mstari 28)?

_____

8. Samsoni aliweka mikono yake katika nguzo mbili za katikati ya hekalu. Maneno yake ya mwisho yalikuwa nini?

_____

a. Alisukuma kwa nguvu zake zote _____

b. Ni aki na nani waliofariki pamoja naye?

_____

9. Tunaambiwa nini katika mstari wa 31? _

_____

Sehemu 5

KUTAFAKARI: Viongozi wa Wafilisti walidhani kuwa kisasi cha mwisho kilikuwa ni chao. Walisherekea kwa furaha wakijiamini kuwa mungu wao Dagoni amemweka Samsoni mikononi mwao. Lakini Samsoni aliendelea kutafuta kisasi kwa mara ya mwisho. Katika mstari wa 28 alimwomba Mungu nguvu ya kumfanya afanye msukumo mmoja ambao ungempa kulipa kisasi kwa kupoteza macho yake. Katika hali ya kimwili alikuwa amepoteza macho yake. Mtu anaweza kujiuliza kama alikuwa hajapoteza macho yake ya kiroho. Watu awalikuwa wakila na kusherekea ushindi wao kwa Samsoni kuwa mikononi mwao Walikuwa wakimpa Dagoni sifa

kwa kufanikiwa kwao na walitoa sadaka kubwa kwa huyu mungu wao. Wakiabudu huyu mungu batili, hii haikuwa sababu ya Samsoni kumwita Mungu ili afanye amwezeshe kutenda kitendo kikubwa cha nguvu isiyo ya kawaida. Bali alitaka alipe kisasi Wafilisti kwa kutoboa macho yake.

- Ni jambo gani lililo mfanya Samsoni kupoteza malengo yake? Ni jambo gani lililo mfanya kusahau kuwa Mungu alikuwa amemtenga kwa makusudi matakatifu?

  _____

- Kisasi chake kwa Wafilisti kiliridiidishaje maono yake ya kuona katika mtazamo wa Kimungu? _____

  _____

- Samson kipofu aliona aliweza kuona na kuita kisasi cha Mungu kwa Wafilisti waliokuwa wakisherekea ushindi wa Dagoni ? Thibitisha jibu lako: _____

  _____

Tumia mua kuandika tafakari yako kwa mwisho mbaya wa msiha ya Samsoni kufuatana na mistari hii Waamuzi 16:23-31. _____

_____

SALA: Mungu mwenye nguvu, kwa kupitia maisha ya Samsoni tunaona uharibifu wa kisasi. Mwisho tunaona uharibufu uliotokea, upotevu wa maisha—vifo. Samsoni alipoteza malengo na mwisho anafariki. Ondoa maharibifu ya chuki maishani mwangu yabadilishe na upendo wako wa msamaha. Niwezeshe kuona maisha katka mtazamo wako nisamehe na unipe neema yako na huruma. Siku zote fanya macho yangu kuelekea kwako, mtoaji wa meme yote. Nijaze huruma yako na niwezeshe kuitikia maisha yote na neema na huruma, si kwa kulipa mabaya kwa mabaya bali kulipa mabaya kwa mema.

_____

KITABU CHA WAAMUZI KINAHITIMISHA: Japo hatutaangalia kwa undani sura zilizosalia za kitabu cha Waamuzi, sentesi moja inayojirudia mara nyingi inabakia. Tunaambiwa nini katika Waamuzi 17:6, 18:1, 19:1 and 21:25? _____

_____

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES

Ufisadi ulikuwa umezidi. Juu ya yote, sanamu na vinyago vilitengenezwa, viliabudiwa na kutunzwa kwenye nymba za wana wa Israeli. Zaidi ya hayo manabii walipotoka, walitafuta mambo yao wenyewe badala ya kutafuta mambo ya Mungu Hali ya maisha imefupishwa katika maneno haya: "katika kipindi hicho Israeli walikuwa hawana mfalme; kila mtu alifanya alichoona." Kitabu cha Waamuzi kinahitimisha kwa maneno hayo.

Pasipokutii sheria za Mungu za Israeli walijifanyia sheria zao. Walijitengeneza mungu wao wa kuwaongoza. Sheria yao ilikuwa kuwa hakuna sheria. Walipoteza sifa kama watu wa Mungu. Walijichanganya wakawa sawa na watu wengine. Hawakuishi tena kama watu waliotengwa kwaajili ya Mungu. Waliacha majukumu yao katika jamii na kujiona kama watu binafsi maarufu.

Kumbuka hali ambayo "kila mtu alifanya kama alivyoona" inaweza kubadilishwa na kuleta tofauti:

- Katika jamii? _____
- Katika familia? _____
- Katika nafsi yako?

  _____

MARUDIO

Taja majina ya watu unaowakumbuka katika somo hili. Andika maneno machache yanayohusu watu hao. Usikate tamaa usipoyakumbuka yote. Hili silo zoeze, kwahiyo tazama rejea zinazoweza kusaidia kumbukumbu yako!

Jina	**Maelezo**	**Rejea**
Yoshua		Yoshua 1
Rahabu		Yoshua 2
Akani		Yoshua 7

©2009 FULLVALUE MINISTRIES

Ehudi, Debora, Na Gidioni		Waamuzi 3-6
Mnaziri		Waamuz 13:7
Samsoni		Waamuz 13
Wafilisti		Waamuz 13:1
Delila		Waamuz 16

Sentensi na maneno machache yalirudiwa katika kujifunza kwetu. Orodhesha unayokumbuka. Rejea zimewekwa kukusaidia kuanza.

1. Yoshua 1:6 _____
2. Yoshua 10:28 _____
3. Yoshua 11:23 _____
4. Yoshua 1:19 _____
5. Yoshua 2:11 _____
6. Yoshua 14:19 _____

Andika sentesi tatu au nne kuelezea kilichotokea kwa Israeli katika kitabu cha Yoshusa na Waamuzi. Kulitokea nini kuhusiana na ardhi, uongozi wao, kumilikki ncni, kuishi bila mfalme, kuendelea kupungua maisha yao ya kiroho kwa kuhusianisha kumwabudu Mungu na kuabudu miungu.? _____

_____

 ©2009 FULLVALUE MINISTRIES